# Jinsi COVID-19 inavyoathiri juhudi za kukabiliana na uzalishaji wa gesi chafu

Ripoti ya kukabiliana na pengo la uzalishaji wa gesi chafu ya mwaka wa 2021: Dhoruba inajikusanya

UN environment programme 50 1972-2022

**Wakati dunia inapoweka juhudi za kupunguza uzalishaji wa gesi chafu - juhudi ambazo bado hazitoshi - toleo la sita la Ripoti ya UNEP ya kukabiliana na pengo la uzalishaji wa gesi chafu: Dhoruba Inajikusanya inaonyesha kuwa ongezeko la madhara kwa mazingira yanaendelea kwa kasi sana kuliko juhudi zetu za kukabiliana na hali hiyo. Makala haya yanaangazia jinsi janga la COVID-19 linavyoathiri juhudi za kukabiliana na uzalishaji wa gesi chafu, na jinsi ambavyo kujikomboa na janga hili kunavyoweza kusaidia mataifa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.**

## Ulimwengu unahitaji kuimarisha juhudi za kukabiliana na athari zisizoweza kugeuzika za mabadiliko ya tabianchi.

Ahadi za sasa chini ya Mkataba wa Paris zinaonyesha kutakuwa na ongezeko la joto la nyuzijoto 2.7 duniani kufikia mwishoni mwa karne hii. Hata dunia ikidhibiti ongezeko la joto lisizidi nyuzijoto 1.5 au nyuzijoto 2, kama ilivyoainishwa kwenye mkataba, bado kuna hatari nyingi kwa mazingira. Kukabiliana na hali hii kunaweza kupunguza hatari hizi na gharama zake, zinazoongezeka joto linapozidi kuongezeka.

## Janga la COVID-19 limeathiri, na litaendelea kuathiri juhudi za kukabiliana na pengo.

Janga hili linaongeza hatari kwa kuathiri uwezo wa ulimwengu wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi: jinsi ilivyoshuhudiwa katika vimbunga vya Pasifiki vya mwaka wa 2020, ambapo masharti ya COVID-19 yalizuia juhudi za kukabiliana na majanga. Wakati uo huo, kudorora kwa uchumi, kupoteza kazi na kuongezeka kwa umaskini huathiri vibaya makundi ya watu yaliyo hatarini kuathiriwa na kupunguza zaidi uwezo wao wa kukabiliana na majanga mabaya kwa mazingira. Hatimaye, kuongezeka kwa gharama ya kulipa madeni, pamoja na kupungua kwa mapato ya serikali, vinaweza kuathiri matumizi ya fedha za serikali ya kukabiliana na gesi chafu katika siku zijazo, hasa katika nchi zinazoendelea.



## Fursa ya kutumia hela za kujiimarisha baada ya janga la COVID-19 kukabiliana vyema zaidi na gesi chafu inapotea.

Makadirio ya gharama za kukabiliana na gesi chafu katika nchi zinazoendelea ni kubwa mara tano hadi kumi zaidi kuliko mtiririko wa sasa wa fedha za umma za kukabiliana na hali hii. Wakati uo huo, ni sehemu ndogo tu ya dola za Marekani trilioni 16.7 za bajeti kote ulimwenguni zimetengewa kukabiliana na hali hiyo. Chini ya theluthi moja ya nchi 66 zilizofanyiwa utafiti zimefadhili wazi mikakati ya kukabiliana na COVID-19 ili kushughulikia madhara kwa mazingira kufikia Juni mwaka wa 2021.

## Janga la COVID-19 bila shaka linatoa mafunzo ya kuboresha mikakati na ufadhili wa kushughulikia mazingira na kutoa fursa za kujiimarisha bila kuchafua mazingira.

Serikali zinapaswa:

- Kushughulikia madhara anuai kupitia mbinu zinazoshirikisha udhibiti wa madhara: kama vile tathmini za makundi ya watu walio hatarini zaidi zinazolenga nchi mahususi.
- Kutumia bajeti ya kujikwamua na janga kutoa kipaumbele kwa juhudi zinazokuza uchumi na kuwezesha kustahimili mabadiliko ya tabianchi.
- Kuanzisha mifumo ya ufadhili wa kushughulikia majanga inayoweza kubadilika: ili kuhakikisha kuwa uwepo wa fedha unaweza kutabirika, zitakuwepo na kutumika kikamilifu kukabiliana haraka na matukio yoyote ya dharura.



**Nchi zilizoendelea zinapaswa kusaidia nchi zinazoendelea na fedha ili kuziwezesha kujiimarisha baada COVID-19 kwa kuzipa fedha kwa masharti nafuu na kuzisamahe madeni makuu.**

UNEP DTU PARTNERSHIP
WASP WORLD ADAPTATION SCIENCE PROGRAMME
UN environment programme 50 1972-2022